MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA



JARIDA LA HALI YA HEWA KILIMO

## MUHTASARI

- Mvua zinazotarajiwa kwa baadhi ya maeneo nchini zinaweza kuambatana na vipindi vya ukavu na kuathiri mazao yaliyopandwa.
- Wakulima katika maeneo ya nyanda za juu kaskazini mashariki na pwani ya kaskazini wanashauriwa kupanda mazao kwa kufuata ushauri wa maafisa ugani katika maeneo yao.

## MIFUMO YA HALI YA HEWA KATIKA KIPINDI CHA NOVEMBA 11-20, 2021

Katika dekadi hii migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kusini (St. Helena na Mascarene) iliendelea kupungua nguvu wakati ile iliyopo kaskazini mwa ikweta (Azore na Siberia) iliimarika. Hali hii iliendelea kuusukuma ukanda mvua (ITCZ) kuelekea kusini mwa Ikweta na hivyo kuwa katika baadhi ya maeneo nchini. Joto la bahari la juu kidogo ya wastani lilikuwepo upande wa mashariki mwa bahari na pia joto la wastani upande wa magharibi mwa bahari ya Hindi. Hali hii ilikuwa na mchango mdogo katika kuusukuma upepo wenye unyevunyevu kuvuma kuelekea katika baadhi ya maeneo ya ukanda wa pwani. Joto la bahari la juu ya wastani lilikuwepo upande wa kusini mashariki mwa bahari ya Atlantiki (karibu na pwani ya Angola) na hivyo kuwa na mchango kidogo wa kusukuma upepo uvumao kutoka magharibi mwa misitu ya Congo kuelekea maeneo ya magharibi pamoja na ukanda wa Ziwa Victoria.

## MWENENDO WA MVUA KATIKA KIPINDI CHA NOVEMBA 11-20, 2021

Kwa ujumla, maeneo mengi nchini yalikuwa makavu isipokuwa maeneo machache ya mikoa ya Mara, Simiyu, Mwanza, Kagera, Geita, Arusha, Manyara, Kigoma, Rukwa, Katavi, Songwe na Njombe ambayo yamepata mvua kama inavyoonekana katika Kielelezo




Kielelezo 1: Kiasi cha mvua kwa kipindi cha Novemba 11-20, 2021

## TATHMINI YA HALI YA KILIMO KATIKA KIPINDI CHA NOVEMBA 11-20, 2021

Katika kipindi hiki, wakulima katika maeneo yanayopata mvua mara mbili kwa mwaka wameendelea kupanda mahindi, maharagwe na mihogo kwa kutumia mvua chache zilizonyesha katika maeneo hayo. Wakulima katika maeneo ya kanda ya ziwa waliendelea na shughuli za palizi ya mazao.

Kwa maeneo yanayopata msimu mmoja wa mvua kwa mwaka, wakulima waliendelea na uandaaji wa mashamba kwa ajili ya mvua za msimu.

Upungufu wa maji na malisho kwa ajili ya mifugo umeendelea kuwepo kutokana na hali ya ukavu inayoendelea.

## HALI YA MAJI KATIKA KIPINDI CHA NOVEMBA 11-20, 2021

Katika dikadi hii, kina cha maji katika mabwawa, mabonde na mtiririko wa maji kwenye mito viliendelea kupungua katika maeneo mengi nchini.

## MIFUMO YA HALI YA HEWA INAYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA NOVEMBA 21-30, 2021

Katika dekadi hii migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kusini inatarajiwa kuendelea kupungua nguvu wakati ile iliyopo kaskazini mwa ikweta inatarajiwa kuimarika kidogo. Hali hii inatarajiwa kusababisha ukanda mvua (ITCZ) kusogea kuelekea katika baadhi ya maeneo ya kanda ya Ziwa Victoria na magharibi mwa nchi. Joto la bahari la juu kidogo ya wastani linatarajiwa upande wa mashariki mwa bahari ya Hindi wakati kusini magharibi, joto la bahari linatarajiwa kuwa la wastani. Hali hii inatarajiwa kuendelea kuusukuma upepo wenye unyevunyevu kuvuma kutoka kusini mashariki kuelekea maeneo ya ukanda wa pwani. Joto la bahari la juu kidogo ya wastani linatarajiwa upande wa kusini mashariki mwa bahari ya Atlantiki (karibu na pwani ya Angola) na hivyo kuwa na mchango mdogo katika kuusukuma upepo wenye unyevunyevu kutoka misitu ya Congo kuelekea magharibi mwa nchi. Kwa ujumla, mifumo hii ya hali ya hewa inatarajiwa kusababisha mvua zinazoambatana na ngurumo katika baadhi ya maeneo ya kanda ya ziwa Victoria na magharibi mwa nchi.

## HALI YA HEWA INAYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA NOVEMBA 21-30, 2021

Maeneo ya kanda ya Ziwa Victoria (mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Simiyu na Mara) na magharibi mwa nchi (mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora) yanatarajiwa kuwa na vipindi vya mvua na ngurumo za radi katika maeneo machache.
Nyanda za juu kaskazini mashariki (mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro), pwani ya kusini (mikoa ya Mtwara na Lindi) pamoja na pwani ya kaskazini (mikoa ya Tanga, maeneo ya kaskazini mwa Morogoro, pwani na Dar es Salaam pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba) yanatarajiwa kupata vipindi vichache vya mvua nyepesi katika maeneo machache.
Maeneo mengi ya kanda ya kati (mikoa ya Dodoma na Singida), kanda ya kusini (mkoa wa Ruvuma na maeneo ya kusini mwa Morogoro) na nyanda za juu kusini magharibi (mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe na Iringa) yanatarajiwa kuwa makavu kwa ujumla.

## HALI YA HEWA KILIMO: MATARAJIO NA USHAURI KIPINDI CHA NOVEMBA 21-30, 2021

Mvua zinazotarajiwa kwa baadhi ya maeneo ya nyanda za juu kaskazini na ukanda wa pwani zinaweza kufuatana na vipindi virefu vya ukavu na kuathiri uoteshaji wa mazao katika maeneo hayo. Wakulima katika maeneo haya wanashauriwa kupanda mazao kwa kufuata ushauri wa maafisa ugani katika maeneo yao.

Upungufu wa upatikanaji wa maji na malisho kwa ajili ya mifugo unatarajiwa kutokana na hali ya ukavu inayoendelea katika maeneo mengi nchini.

Wakulima, wafugaji na wavuvi wanashauriwa kupata ushauri zaidi kutoka kwa wataalamu wa sekta husika. Inashauriwa kuendelea kufuatilia utabiri wa hali ya hewa wa kila siku, siku tano na tahadhari kadri zinavyotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa nchini.

## HALI YA MAJI INAYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA NOVEMBA 21-30, 2021

Kina cha maji katika mabwawa na mtiririko wa maji kwenye mito vinatarajiwa kuendelea kupungua katika maeneo mengi nchini kutokana na hali ya ukavu inayoendelea.
Hivyo, wananchi na mamlaka husika wanashauriwa kutumia rasilimali maji kwa uangalifu.

*Jarida limetayarishwa na:*
**Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania**
**Ghorofa ya 3 -Ubungo Plaza – 388 Barabara ya Morogoro,**
***S.L.P 3056; 16102 Dar es Salaam, Simu. 255 -(0) 22 – 2460706-8; Nukushi: 255 - (0) 22 – 2460718 ; Barua pepe: (1) met@meteo.go.tz (2) agromet@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz***, -Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania